



TANGAZO

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza miti laini na migumu katika mashamba 11 ya miti ya kupanda yanayomilikiwa na Serikali kwa msimu wa uvunaji wa mwaka wa fedha 2023/2024.

Tathmini iliyofanyika 2023/24 inaonesha bado kuna upungufu wa malighafi itakayogawanywa kwa viwanda vilivyosimikwa kutoka katika baadhi ya mashamba (Jedwali 1) ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya viwanda hivyo. .

Jedwali 1: Orodha ya mashamba ya miti yenye upungufu wa malighafi na jamii ya miti itakayovunwa kwa msimu wa uvunaji wa 2023/2024.

Na.	Jina la Shamba	Anwani	Mahali lilipo	Aina ya miti
1	Meru / Usa	S.L.P 1257, Arusha	Arumeru, Arusha	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus patula</i>),• Mikaratusi (<i>Eucalyptus spp</i>),• Mkavelia (<i>Grevillea robusta</i>),
2	Buhindi	S.L.P 1480, Mwanza	Sengerema, Mwanza	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus caribaea</i>).
3	North Kilimanjaro (Rongai)	S.L.P 40, Tarakea	Rombo, Kilimanjaro	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus patula</i>),• Mikaratusi (<i>Eucalyptus spp</i>),
4	West Kilimanjaro	S.L.P 161, Hai	Hai, Kilimanjaro	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus patula</i>),• Mikaratusi (<i>Eucalyptus spp</i>)• <i>Cupressus lusitanica</i> na• <i>Grevillea robusta</i>
5	Kawetire	S.L.P 770, Mbeya	Mbeya	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus patula</i>), na• Mikaratusi (<i>Eucalyptus maidenii</i>)
6	Kiwira	S.L.P 99, Rungwe	Rungwe, Mbeya	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus patula</i>)
7	Rubare	S.L.P 930, Bukoba	Bukoba, Kagera	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus tecunumanii</i>)
8	Rubyia	S.L.P 134, Nansio	Ukerewe, Mwanza	<ul style="list-style-type: none">• Misindano (<i>Pinus tecunumanii</i>)

Kwa mashamba yenyne malighafi ya ziada (Jedwali Na. 2), mgao utafanyika kulingana na vigezo vitakavyowekwa ikiwemo uwezo wa viwanda vilivyosimikwa na ziada itagawanywa kwa waombaji wapya.

Jedwali 2: Orodha ya mashamba ya miti yenyne malighafi ya ziada na jamii ya miti itakayovunwa kwa msimu wa 2023/2024.

Na	Jina la Shamba	Anwani	Aina ya miti
1	Sao Hill	S.L.P 45, Mafinga, Iringa.	<ul style="list-style-type: none">Misindano (<i>Pinus patula</i>), naMikaratusi (<i>Eucalyptus spp</i>).
2	Shume	S.L.P 60, Lushoto, Tanga.	<ul style="list-style-type: none">Misindano (<i>Pinus patula</i>),<i>Cupressus lusitanica</i>, naMikaratusi (<i>Eucalyptus spp</i>)
3	Ukaguru	S.L.P 2, Gairo, Morogoro.	<ul style="list-style-type: none">Misindano (<i>Pinus patula & Pinus caribaea</i>), naMikaratusi (<i>Eucalyptus spp</i>).

Hivyo, wamiliki wa viwanda ambao wana nia ya kuendelea na uvunaji wanashauriwa kuwasilisha maombi ya kupatiwa malighafi kwa kujaza fomu ya maombi ya uvunaji wa miti na kuyatuma kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti husika. Aidha, kwa waombaji wapya, wanashauriwa kuwasilisha maombi yao kwa Wahifadhi Wakuu wa mashamba ya miti yenyne ziada ya malighafi kama yalivyoainishwa katika Jedwali Na. 2. Fomu za maombi zinapatikana katika ofisi za Wahifadhi Wakuu wa mashamba husika na pia katika tovuti ya Wakala (www.tfs.go.tz). Mwisho wa kupokea maombi ya uvunaji wa miti ni **Jumanne, Juni 27, 2023**, saa 9:30 alasiri.

NB: Mwombaji anapaswa kufika ofisi za Shamba akiwa na kitambulisho cha Taifa au Leseni ya udereva au Pasi ya kusafiria.

Limetolewa na:

**KAMISHNA WA UHIFADHI
S. L. P. 40832
DAR ES SALAAM**